



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

BARAZA LA SANAA LA TAIFA (BASATA)



FOMU YA UHAKIKI WA NYIMBO

Taarifa za wimbo

1. **Jina la msanii:** Nay wa Mitego
2. **Jina la wimbo:** Nitasema
3. **Jina la Mtozi:** Chiby beats
4. **Tarehe ya Kutoka:** 24/09/2024

Daraja la wimbo

WW (U)	WM13(U13)	WM16(U16)	WZ18 (A)	MM (SS)	KK (R)	X
					✓	

Moani ya Mhakiki

Wimbo huu wa msanii Emmanuel Elibariki (Nay wa Mitego) umekiuka Kanuni ya 25, kifungu cha sita, vipengele **C** na **D** vya Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA). Maneno kama “**Wanaokuja kututeka, wanakuja kama polisi.**” na “**Na mkikosea, tukikosea, mnatutumia polisi**” na maneno mengine yanayofanana na hayo hayana ushahidi wa kuthibitisha hilo alilolisema msanii huyo. Hivyo, wimbo huo umekiuka vipengele hivyo vya Kanuni ya 25, kifungu cha 6.

Kutokana na kanuni za BASATA, wimbo wa Nitasema umepewa daraja la **KK** sawa na **R**, kumaanisha kwamba kazi hii ya sanaa imekataliwa kutumika kwa namna yoyote ile.

ANGALIZO:

Wimbo huu usiendelee kufanyiwa matangazo (promotion), usipigwe kwenye vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kutokana na kuwepo kwa maneno hayo yenye ukakasi.

Saini ya Mhakiki


KEFA MAHENGE
AFISA SANAA

TAREHE 24/09/2024


Kevin Matungwa Stansilaus
KAIMU MKURUGENZI SEHEMU YA MUZIKI

MCHANGANUO WA KANUNI YA 25

Kanuni ya 25 Kifungu cha 6 Inaeleza kuwa Ili wimbo uweze kukubalika na kupelekwa kwenye jamii unatakiwa uwe na vitu vifuatavyo

- a) Hauvunji heshima ya mwimbaji, msikilizaji na mtazamaji.
- b) Hauna upotoshaji wa aina yeyote.
- c) Hauchochei ghasia ya aina yoyote au namna yoyote.
- d) Hauna meneno ya uongo, uchochezi au yanayo kashifu watu wengine.
- e) Hauudhurishi lugha chafu na matusi,
- f) Hautukuzi ubaguzi wa rangi, ukabila au dini.
- g) Haukashifu Taifa la Tanzania au mataifa mengine.
- h) Haudhoofishi umoja, ushirikiano na ustawi bora wa jamii.
- i) unazingatia masharti ya sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika masuala ya haki za ubunifu na mambo mengine yote.
- j) Haishawishi wala kuhamasisha vitendo vya ngono, ushoga, usagaji au matumizi ya dawa za kulevya.

MHANGANUO WA MADARAJA YA KAZI ZA SANAA

Na.	DARAJA	UMRI WA HADHIRA WANAO RUHUSIWA	MAELEZO
1.	“WW” sawa na “U”	Watu wote	-
2.	“WM 13” sawa na “U13”	Watoto wa kuanzia umri wa miaka 13 na kuendelea.	-
3.	“WM 16” sawa na “U16”	Watoto sawa na umri wa kuanzia miaka 16 na kuendelea.	-
4.	“WZ18” sawa na “A”	Watu wa umri kuanzia miaka 18 na kuendelea.	-
5.	“MM” sawa na “SS”	Maonesho maalum	Maonesho ya kielimu au mafunzo.
6.	“KK” sawa na “R”	Kukataliwa kazi ya Sanaa Pamoja na matumizi yake kwa namna yoyote	Kazi ya Sanaa haitaruhusiwa kusambazwa kwa namna yoyote.
7.	“X”	Hairuhusiwi kuoneshwa mahali popote nchini	Muhusika atakamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria.